**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# RISALA YA MWENYEKITI WA TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI KUHUSU UCHAGUZI MKUU UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMATANO

**TAREHE 29 OKTOBA, 2025**

***Ndugu wananchi,***

Kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 38(2)(a), 65 na 74(6) (b) na (d) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ikisomwa pamoja na kifungu cha 49 na 58(2) vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza Ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025.

Kwa mujibu wa Ratiba hiyo, mwisho wa kampeni za uchaguzi kwa Tanzania Bara ni tarehe 28 Oktoba, 2025 saa kumi na mbili kamili (12:00) jioni na kwa Tanzania Zanzibar itakuwa tarehe 27 Oktoba, 2025 saa kumi na mbili kamili (12:00) jioni ili kupisha kura ya mapema. **UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA MADIWANI KWA TANZANIA BARA UTAFANYIKA SIKU YA JUMATANO TAREHE 29 OKTOBA, 2025.**

***Ndugu wananchi,***

Kifungu cha 54 na 66 vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, vimeweka masharti kwamba, katika maeneo yote ambayo yupo mgombea pekee wa Ubunge au Udiwani atapigiwa kura ya ndiyo au hapana.

Tume imeandaa karatasi za kura kwenye majimbo au kata zenye mgombea pekee. Karatasi hiyo itakuwa na nembo na jina la chama cha mgombea, picha ya mgombea na majina yake na kulia kwa kararatasi kuna visanduku viwili, kisanduku kimoja kimeandikwa **"ndiyo"** na kisanduku kingine kimeandikwa "**hapana"**.

Hivyo, mpiga kura atakayefika kituo cha kupigia kura kwenye jimbo au kata ambayo ina mgombea pekee, atapewa karatasi ya kura ya mgombea pekee na atapiga kura kwa

kuweka alama ya vema kwenye kisanduku cha “**ndiyo”** kuonesha amemchagua mgombea au ataweka alama ya vema kwenye kisanduku cha **“hapana”** iwapo hakumchagua mgombea.

***Ndugu wananchi,***

Napenda kurudia kwamba, upigaji kura ya “**ndiyo”** au **“hapana”** utahusisha majimbo au kata ambazo zina mgombea pekee wa ubunge au udiwani. Aidha, taratibu zingine za upigaji kura kwenye majimbo na kata zitakuwa kama kawaida.

***Ndugu wananchi,***

Napenda kutumia nafasi hii, kuvipongeza Vyama vya Siasa na wagombea waliojitokeza na walioteuliwa kugombea nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Ubunge na Udiwani. Kwa namna ya kipekee nivipongeze vyama vyenye wagombea, wagombea wao, wanachama, wapenzi, wafuasi na mashabiki wao kwa kufanya kampeni za kistaarabu na kuzingatia Kanuni za Maadili ya Uchaguzi za Mwaka 2025.

Aidha, nawapongeza wananchi wote, kwa utulivu mliouonesha wakati wote wa kipindi cha kampeni. Kwa kiasi kikubwa kampeni zimefanyika kwa utulivu na amani na pale palipojitokeza kasoro ndogondogo katika kampeni hizo, Kamati za maadili katika kila ngazi zilishughulikia malalamiko hayo kwa ufanisi mkubwa.

***Ndugu wananchi,***

Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 jumla ya wapiga kura **37,647,235** wanatarajiwa kupiga kura, ambapo kati ya hao, wapiga kura **36,650,932** wapo Tanzania Bara na wapiga kura **996,303** wapo Tanzania Zanzibar. Aidha, wapiga kura wanawake ni **18,950,801** sawa na asilimia **50.34** na wanaume ni **18,696,434** sawa na asilimia **49.66**.

Jumla ya majimbo yote ya Jamhuri ya Muungano ni **272,** ambapo kwa Tanzania Bara yapo **222** na Tanzania Zanzibar yapo **50.** Aidha, Kata kwa ajili ya uchaguzi wa Madiwani Tanzania Bara zipo **3,950.**

Kwa uchaguzi wa wabunge, majimbo **270** ndio yatakayofanya uchaguzi wa Wabunge, na majimbo mawili (02) ya Fuoni Tanzania Zanzibar na Siha kwa Tanzania Bara, hayatafanya uchaguzi kwa kuwa ratiba yake ilibadilika kutokana na vifo vya wagombea. Uchaguzi katika majibo hayo utafanyika tarehe 30 Desemba, 2025.

Kwa upande wa uchaguzi wa madiwani kwa Tanzania Bara, kata 3,945 ndizo zitakazofanya uchaguzi wa udiwani tarehe 29 Oktoba, 2025, wakati kata tano (05) ambazo ni Chamwino – Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Mbagala Kuu – Halmashauri ya Manispaa ya Temeke  na Nyakasungwa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, hizi zitafanya uchaguzi wa udiwani tarehe 30 Desemba, 2025.

Kata zingine ni Mindu  - Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro na Kata ya Mzinga Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam ambazo zitafanya uchaguzi wa udiwani tarehe 05 Januari, 2026.

***Ndugu wananchi,***

Kwa mara ya kwanza na kwa mujibu wa Ibara ya 5(3)(d) ya Katiba ikisomwa pamoja na kifungu cha 42(3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume imetoa fursa kwa wapiga kura kuomba kupiga kura ya Rais katika vituo vya kupigia kura tofauti na vituo walivyojiandikisha ambapo jumla ya wapiga kura **8,277** waliomba na kukubaliwa kupiga kura ya Rais katika vituo tofauti na vituo walivyojiandikisha.

Aidha, kwa kuzingatia kifungu cha 10(1)(c) cha Sheria rejewa, kwa mara ya kwanza, wafungwa kwa Tanzania Bara na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo kwa Tanzania Zanzibar wanaotumikia kifungo kwa kosa ambalo adhabu yake haizidi miezi sita na mahabusu wataruhusiwa kupiga kura ya Rais. Hivyo, vituo **129** vya magereza kwa Tanzania Bara na vituo kumi na moja (**11**) kwa Vyuo vya Mafunzo kwa Tanzania Zanzibar vitatumika kupiga kura kwa wafungwa, wanafunzi na mahabusu.

***Ndugu wananchi,***

Jumla ya vituo vya kupigia kura **99,895** vitatumika, kati ya hivyo, vituo **97,348** vipo Tanzania Bara na vituo **2,547** vipo Tanzania Zanzibar.

Katika uchaguzi huu, vyama vya siasa **17** vimesimamisha wagombea katika nafasi ya Kiti cha Rais na Makamu wa Rais na vyama **18** vimesimamisha wagombea wa Ubunge na Udiwani.

Wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais ni **17**, ambapo kati yao wagombea wa Kiti cha Rais watatu **(03)** sawa na asilimia **17.65** ni wanawake na wagombea kumi na nne **(14)** sawa na asilimia **82.35** ni wanaume.

Kwa upande wa wagombea wa kiti cha Makamu wa Rais wapo **17**, kati yao wagombea tisa **(9)** sawa na asilimia **53** ni wanawake na wagombea nane **(8)** sawa na asilimia **47** ni wanaume.

***Ndugu wananchi,***

Jumla ya wagombea **1,729** wanawania nafasi za ubunge, ambapo kati yao wagombea wanawake ni **558**, sawa na asilimia **32** ya wagombea na wanaume ni **1,171**, sawa na asilimia **68** ya wagombea ubunge nchi nzima na wagombea wenye ulemavu ni **27**, sawa na asilimia **1.56** ya wagombea wote wa ubunge.

Kwa upande wa wagombea wa nafasi ya udiwani wapo **7,239**, ambapo kati yao wagombea wanawake ni **718**, sawa na asilimia **10** na wanaume ni **6,521**, sawa na asilimia **90** ya wagombea udiwani Tanzania Bara. Aidha, watu wenye ulemavu ni **57**, sawa na asilimia **0.79** ya wagombea udiwani wote.

***Ndugu wananchi,***

Kwa upande wa maandalizi, Tume imekamilisha maandalizi yote muhimu ya uchaguzi, ikiwemo usambazaji vifaa katika maeneo ya uchaguzi. Hadi kufikia leo, vifaa vyote vimefikishwa kwenye maeneo husika ambapo usambazaji wa vifaa hivyo kwenda kwenye vituo vya kupigia kura unaendelea. Aidha, uteuzi na uendeshaji wa mafunzo kwa watendaji wa vituo vya kupigia kura umefanyika na kukamilika.

***Ndugu wananchi,***

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 4, 14(2), 19(3), 84(3)(a) na (b) na 164 vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 na kifungu cha 26 cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, pamoja na kuwezesha wananchi walioandikishwa na ambao wamepata changamoto kuhusu kupiga kura, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatoa Maelekezo ya Kisera Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 kama ifuatavyo:-

(i) kwa mpiga kura asiye na picha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lakini ana kadi ya mpiga kura yenye taarifa binafsi zilizomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, **ATARUHUSIWA KUPIGA KURA;**

(ii) kwa mpiga kura ambaye ana kadi yenye namba ya mpiga kura inayotofautiana na namba ya mpiga kura iliyomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lakini taarifa nyingine zote ikiwemo picha na majina yaliyopo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ni sawa kama ilivyo katika kadi ya mpiga kura aliyonayo, **ATARUHUSIWA KUPIGA KURA;**

(iii) kwa mpiga kura ambaye ameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na taarifa zake zipo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililopo katika kituo husika, lakini amepoteza kadi yake au kadi yake imeharibika, **ATARUHUSIWA KUPIGA KURA** kwa kutumia mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo:

a) Kitambulisho cha Taifa (NIDA);

b) Leseni ya udereva; au

c) Pasi ya kusafiria (*Passport*)

Lakini kwa sharti kwamba, majina yake yaliyopo katika kitambulisho atakachowasilisha mpiga kura, ni lazima yafanane na majina yote kama yalivyo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

(iv) kwa mpiga kura ambaye ana kadi ya kupigia kura lakini taarifa zake hazipo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura **HATARUHUSIWA KUPIGA KURA**; na

(v) kwa wapiga kura wote kutoka katika kata 10 zilizofutwa ambazo ni Kata ya Kanoge, Litapunga, Katumba, Mtapenda (Kijiji cha Ikolongo na Ndurumo) vilivyopo katika Jimbo la Nsimbo, Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo. Kata ya Mishamo, Ilangu, Bulamata na Ipwaga zilizopo katika Jimbo la Tanganyika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika Mkoani Katavi na Kata ya Milambo, Igombemkulu na Kanindo zilizopo katika Jimbo la Ulyankulu Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua Mkoani Tabora ambazo wapiga kura walihamishiwa katika kata za jirani lakini kadi zao zinaendelea kusoma taarifa za awali za vituo vyao vya

zamani vilivyofutwa, **WATARUHUSIWA KUPIGA KURA KATIKA VITUO VIPYA WALIVYOHAMISHIWA**.

***Ndugu wananchi,***

Kabla sijahitimisha risala yangu, napenda kuwakumbusha na kusisitiza yafuatayo:

(i) siku ya uchaguzi ni tarehe 29 Oktoba, 2025. Siku hiyo vituo vya kupigia kura vitafunguliwa saa moja kamili (1:00) asubuhi na vitafungwa saa kumi kamili (10:00) alasiri.

Kwa upande wa vituo vya kupigia kura vya Magereza na Vyuo vya Mafunzo, vituo vitafunguliwa saa mbili kamili (2:00) asubuhi na kufungwa saa tisa kamili (9:00) alasiri.

Hata hivyo, mpiga kura yeyote atakayekuwepo kwenye mstari kituoni wakati wa kufunga kituo ataruhusiwa kupiga kura. Aidha, ifikapo muda wa kufunga kituo mlinzi wa kituo atasimama nyuma ya mpiga kura wa mwisho kwenye mstari ili kuhakikisha kwamba mpiga kura anayepiga kura ni yule aliyefika ndani ya muda uliobainishwa. Zoezi la upigaji kura litaendelea hadi wapiga kura wote watakapomalizika.

(ii) Hairuhusiwi kuvaa sare za chama cha siasa kwenye vituo vya kupigia kura, kuendesha kampeni za uchaguzi au kukaa ndani ya mita mia tatu **(300)** kutoka eneo la kupigia kura Siku ya Uchaguzi.

(iii) Iwapo mpiga kura atafika kituoni na kushindwa kutambua kituo chake cha kupigia kura, atasaidiwa na karani mwongozaji wapiga kura kwa kutafuta jina lake kwenye orodha na kumwelekeza kituo cha kupigia kura kilipo.

(iv) Wapiga kura waliosimama kwenye mstari wanapaswa kutoa kipaumbele kwa watu wenye mahitaji maalum kama vile **wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wanaonyonyesha ambao wamekwenda na watoto wao vituoni**.

(v) Wapiga kura wenye ulemavu wa kutoona lakini wana ufahamu wa kusoma maandishi ya nukta nundu, watapewa fursa ya kutumia Jalada la Nukta Nundu (Tactile Ballot Folder) ili waweze kupiga kura wenyewe. Kwa

wasioweza kutumia jalada hilo, wataruhusiwa kwenda vituoni na watu waliowachagua wenyewe ili kuwasaidia kupiga kura.

(vi) Kwa mujibu wa kifungu cha 84(3)(e) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 upigaji kura ni wa siri, hivyo kila mtu apige kura yake kwa siri na mtu asishawishiwe na mtu yeyote kueleza ni nani amempigia kura.

(vii) Mara baada ya kupiga kura, wapiga kura wanatakiwa kuondoka vituoni na kurejea nyumbani. Kwa kuwa Vyama vya Siasa vitakuwa vimeweka mawakala wao vituoni, maslahi ya vyama na wagombea yatalindwa na mawakala wao.

(viii) Kwa kuzingatia kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, mpiga kura atapiga kura kwenye kituo chake alichojiandikisha au alichopangiwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

(ix) Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 5(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 42(3) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2024 na kanuni ya 48(1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, mpiga kura yeyote ambaye alihamisha taarifa zake kwenda kwenye kituo ambacho hakujiandikisha na ambacho aliomba kupiga kura ya Rais pekee **HATARUHUSIWA KUPIGA KURA** katika kituo alichokuwa amejiandikisha kwa kuwa jina lake **halitaonekana** kwenye kituo alichojiandikisha kwa Siku ya Uchaguzi **tarehe 29 Oktoba, 2025**.

(x) Baada ya upigaji kura kukamilika, zoezi la kuhesabu kura litafanyika katika kituo ambacho upigaji kura umefanyika, au yakitokea mazingira yenye changamoto, zoezi la kuhesabu kura linaweza kufanyikia kwenye eneo lingine.

(xi) Ifahamike kuwa mawakala wa vyama vya siasa watakuwepo kushuhudia zoezi la kutangaza matokeo katika vituo vya kujumlishia kura kwenye ngazi ya kata, jimbo na Makao Makuu ya Tume kuanzia hatua ya kujumlisha matokeo na hatimaye kumtangaza mshindi.

*Ndugu wananchi,*

Kwa kumalizia na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Tume na Menejimenti ya Tume navitakia kila la kheri vyama vya siasa na wagombea wanaoshiriki kugombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Ubunge na Udiwani.

Ninawasihi wadau wote wa uchaguzi na wananchi kwa ujumla kuweka uzalendo mbele kwa maslahi mapana ya Taifa letu kwa kuwa sote tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa amani ya nchi yetu inaendelea kuwepo na hatimaye kuwa na uchaguzi huru, wa haki na wa kuaminika. Jambo hili litawezekana iwapo kila mdau atatimiza haki na wajibu wake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu.

Kwa mara nyingine natoa rai kwa wapiga kura wote nchini kujitokeza kwa wingi **Siku ya Jumatano ya tarehe 29 Oktoba, 2025** katika vituo vya kupigia kura ili kuwachagua viongozi wanaowataka wawaongoze kwa kipindi cha miaka mitano (5) ijayo.

**"KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA"**

Imetolewa tarehe 27 Oktoba, 2025; na

Jaji (Rufaa) Jacobs C.M. Mwambegele

**MWENYEKITI**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura